

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA TATU

Kikao cha Hamsini na Tisa- Tarehe 25 Juni, 2021

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Spika (Mhe. Job Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Tunaendelea na Mkutano wetu wa Tatu leo ni Kikao cha Hamsini na Tisa. Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, ndc – KATIBU WA BUNGE:**

### MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Maswali, tutaanza na Mheshimiwa Askofu Josepat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe.

Na. 490

**Kuzipandisha hadhi Barabara za Jimbo la Kawe**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA aliuliza:-**

Je, Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka wa kuzipandisha hadhi barabara za ndani za Jimbo la Kawe ili zihudumiwe na *TANROADS* kwa kuwa uwezo wa *TARURA* kuhudumia ni kilometra 120 wakati Jimbo lina barabara zenye jumla ya kilometra 1,463?

**SPIKA:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la kupandisha hadhi barabara ni la kisheria na huzingatia vigezo viliviyowekwa kwa mujibu wa Sheria ya Barabara Namba 13 ya mwaka 2007 na Kanuni zake za mwaka 2009. Barabara ambayo inakidhi vigezo vya kupandishwa hadhi inatakiwa ijadiliwe kwenye Kikao cha Bodi ya Barabara ya Mkoa husika na ikionekana inakidhi vigezo vyote Bodi ya Barabara ya Mkoa husika itamshauri Waziri mwenye dhamana na barabara kuwa barabara husika imekidhi vigezo vya kuwa na hadhi ya barabara ya Mkoa na hivyo ipandishwe daraja na kuwa barabara ya Mkoa chini ya Wakala wa Barabara Tanzania kwa maana *TANROADS*. Hivyo, ni vema taratibu hizo zikafuatwa ili kupandisha hadhi barabara zilizopo katika Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuongezea bajeti *TARURA* ili kuiwezesha kuzihudumia barabara zake ikiwemo kuongeza tozo kwenye mafuta katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 itakayowezesha *TARURA* kupata fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara.

**SPIKA:** Mheshimiwa Askofu Gwajima nimekuona.

**MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Jimbo la Kawe lina barabara nyingi sana ambazo zinaunganisha Wilaya na Wilaya kwa mfano, Wilaya ya Ubungo pamoja na Kindondoni huko kwa juu.

Ni lini sasa Waziri atakwenda pamoja nami ili ukaone hali halisi katika Jimbo hilo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Jimbo la Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mara baada ya Bunge nitaongozana na wewe pamoja na wale Wabunge ambao niliahidi katika Mkoa wa Dar es Salaam kuzungukia barabara zote za Mkoa huo, ahsante. (*Makofii*)

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata ambalo bado liko TAMISEMI la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe.

Na. 491

#### **Kutambuliwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio**

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Je, ni lini Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio itatambuliwa rasmi na kuanza kuwashudumia wananchi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri - TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Jimbo la Ukerewe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tangazo la kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio lilitolewa tarehe 1/10/2007 na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa, Mamlaka za Wilaya Sheria Na. 7 ya mwaka 1982 kifungu cha 16 na 17.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali iliunda timu ya wataalam kwa ajili ya kuchukua maoni ya wananchi kuufanya Mji Mdogo wa Nansio kuwa Halmashauri ya Mji. Wananchi wa kata kumi zilizopendekezwa kuunda Halmashauri ya Mji Nansio waliridhia Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji na mapendekezo hayo yaliwasilishwa Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilipokea mapendekezo hayo na kutuma timu ya wataalam kwenda katika Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio ili kujiridhisha kama vigezo muhimu vinavyotakiwa ili kupandisha hadhi Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio vimefikiwa. Timu ilibaini kuwa Mamlaka ya Mji Mdogo Nansio bado haikidhi vigezo vya kupandishwa hadhi na kuwa Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Spika, vigezo zilivyokosekana ni pamoja na kutokuwa na idadi ya watu angalau 150,000, kutokuwa na eneo lenye ukubwa wa walau kilomita za mraba 300, kutokuwa na kata walau 12 na mitaa 60. Hivyo, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliishauri Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kuendelea kuilea Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nansio mpaka itakapokidhi vigezo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mkundi nimekuona.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nishukuru kwa majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli TAMISEMI walituma timu ikaja kufanya mapitio lakini tokea wakati ule tayari vile vigezo vyote viwili vilivyoonekana havijafikiwa kwa maana ya idadi ya kata ziko kata 12 na idadi ya watu ambacho ni kigezo namba mbili tayari mamlaka ile ina watu zaidi ya 200,000 ni zaidi ya kigezo ilichowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, swali langu sasa, je, Serikali kuitia Ofisi ya Rais - TAMISEMI, wako tayari sasa kuridhia kuifanya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Nansio kuwa halmashauri ya mijini? Nashukuru sana.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri huo mji unaitwa Nasho siyo Nansio.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MITAA NA SERIKALI ZA MITAA (DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mkundi, Mbunge wa Ukerewe kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimejibu kwenye swali la msingi kwamba kwa wakati huo wakati tadhimini inafanyika Nansio ilikuwa haijafikia vigezo viliviyokuwa vinahitajika, lakini kwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa tumeshafikia vigezo hivyo naomba tulichukue jambo hili kama Serikali tukalifanyie tathimini, lakini pia tukajiridhishe kama vigezo hivyo vimefikiwa ndipo tuweze kuona hatua zinazofuata kwa ajili ya kufanya maamuzi. Nakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, nimekuona Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuwa Mji Mdogo wa Namanyere tulishakidhi vigezo na taarifa ziko ofisini kwenu; ni lini sasa mtachukua

hatua kwa mujibu wa sheria ili na sisi tuweze kupata Halmashauri ya Mji?

**SPIKA:** Jamani hata Namanyere nayo iwe mji. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Namanyere nayo kule Kirando iwe mji.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Aida Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi taratibu za kupandisha Mamlaka za Miji Midogo kwenda kuwa Halmashauri za Miji zina utaratibu wake, lakini zina sheria yake na hivyo Serikali siku zote inafanya tathimini kuona kama vigezo vimefikiwa na baada ya hapo hatua stahiki zinachukuliwa.

Kwa hiyo, nimuhidi Mheshimiwa Mbunge kwa taarifa aliyoitoa Serikali pia tutakwenda kupidia vigezo vya Halmashauri kwa maana ya Mji Midogo wa Namanyere na kama umekidhi vigezo Serikali itachukua hatua kwa mujibu wa taratibu. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante tuendelee sasa tuondoke TAMISEMI, twende Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, swalii la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini.

Na. 492

### **Hitaji la Bima ya Afya kwa Wazee**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawapatia wazee hasa wa vijijini bima ya afya ikiwemo ya *CHFinayotolewa* na Halmashauri?

**SPIKA:** Majibu ya swali hiloMheshimiwa Naibu Waziri Afya, Dkt. Godwin Oloyce Mollel, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijiini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, huduma za tiba ni haki ya msingi ya wazee wote. Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa matibabu hususan kwa wazee wasiojiweza nchini kwa kuanzisha madirisha kwa ajili ya matibabu kwa wazee. Serikali imeendelea na zoezi la utambuzi wa wazee na kuwapatia vitambulisho vya matibabu. Hadi kufikia Machi, 2021 jumla ya wazee 2,344,747 wametambuliwa sawa na asilimia 87 ya makadirio ya wazee wote nchini. Kati yao wanaume ni 1,092,310 na wanawake ni 1,252,437. Aidha, wazee wasio na uwezo 1,087,008 na wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bure na wazee 856,052 wamepatiwa kadi za matibabu za Afya ya Jamii yaani CHF.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na kukamilisha rasimu ya Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote ili kuwezesha wananchi wote wakiwemo wazee kupata huduma za matibabu bila kikwazo cha fedha kwa mfumo rasmi na ulio mzuri zaidi. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shamsia.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali inawaambia nini wananchi hasa wazee wenyе kadi za Bima ya Afya pindi wanapokwenda kupata huduma na kujibiwa dawa wakanunue madukani; nini majibu ya Serikali juu ya hili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kutokana na ongezeko kubwa la zahanati vijijini changamoto kubwa ni upatikanaji wa dawa, vifaa tiba kwa maana ya vipimo na waganga. Nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha vifaa hivi vinapatikana bila usumbufu?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Afya, Dkt. Godwin Mollel, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Spika, ni kweli *concern* ya Mbunge anayoisema ndio *concern* kubwa ambayo imeonekana kwenye eneo la *CHF* ambayo wananchi wengi wamekuwa wakienda na wakifika kwenye kituo wanakutana na tatizo hilo la upatikanaji wa dawa pamoja na daktari kumwandikia na *CHF* ni kwamba haiwezi kumsaidia mtu huyu kupata kwenye maduka mengine dawa zaidi ya kwenye kituo husika.

Mheshimiwa Spika, ndio maana sasa hivi Serikali umesikia moja; Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ametoa zaidi ya shilingi bilioni 123 kwa ajili ya kuboresha eneo la dawa, maana yake sasa wakienda vituoni watakutana na dawa. Lakini umemsikia Waziri wetu kwa sababu suala la upatikanaji wa dawa vituoni ni zaidi tu ya fedha zenyewe kupatikana ndio maana umemsikia Waziri wetu wa Afya pamoja na Waziri wa TAMISEMI wameanza kufanya kazi kubwa sana kwenye eneo la uadilifu kuhakikisha kuna *accountability* kwenye eneo zima la dawa. Kwa hiyo hilo ndilo jibu la swali lako la kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili ni upatikanaji vilevile wa dawa na vifaa tiba vituoni; nalo linajibwa na swali la kwanza kwa sababu tukishakuwa na shilingi bilioni 123 ambayo Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan ameshazitoa kimsingi tutakuwa tumetatuwa hilo tatizo. Lakini vilevile sasa tunapokwenda kwenye Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote maana yake hata tukiingia watu wote wakapata bima ya afya inayofanana na hizi ambazo wafanyakazi wa Serikali wanazo hata kama watakosa dawa kwenye kituo chake,

kuna maduka ya dawa ambayo yanatumia Bima ya Afya ambayo ni hii kubwa ya Taifa kwa hiyo tatizo hilo la dawa litaondoka.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mtaturu nilikuona.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Mheshimiwa Waziri katika jibu lake amesema kwamba wanaruhusu kuwahakiki wazee na kwa sababu mfumo wa kuhakiki wazee haujawa rasmi, mmewaachia Halmashauri na ndiyo unakwamisha wazee wengi kutokupata huduma hii kwa kigezo cha kutokusajiliwa.

Ni nini hatua ya ziada ya Serikali kuhakikisha wazee wote wanajiliwa katika muda ambao umepangwa ili wapate haki yao ya matibabu? (*Makofii*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tuelewane na kinachosema Serikali, siyo kusajili wazee wote, kuna wazee kama wa Kisukuma, wa Kinyamwezi ndiyo wanaoa vigoli wadogo, wale hawahuksiki, ni wazee wasiojiweza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO (MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL):** Mheshimiwa Spika, labda nijibu swali zuri la Mheshimiwa Mbunge, moja; nachukua *concern* yake kwa sababu ameonesha kuna tatizo kwenye eneo zima la utambuzi wa wazee. Kwa hiyo tutaenda kukaa kuona ni namna gani tunaweza kuboresha hilo eneo hasa la utambuzi wa kujua ni nani mzee na nani siyo mzee.

Lakini kwa sababu tunakwenda, suala hapa ni tiba ni *ku-access* tiba tunapokwenda kwenye Muswaada wa Bima ya Afya kwa Wote kimsingi hilo litakuwa lipo *contained* kwenye utaratibu mzima, kwa hiyo, halitakuwa tatizo.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee na Ujenzi na Uchukuzi swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mheshimiwa Mhandisi Ulenge, Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa niaba ya Mheshimiwa Mwanaisha.

Na. 493

### **Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege - Tanga**

**MHE. CECILIA PARESSO K.n.y. MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, ni lini ahadi ya upanuzi wa Uwanja wa Ndege Tanga aliyoitoa Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Bomba la Mafuta pale Chongoleni Mkoani Tanga itaanza kutekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, tafadhali.

**WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha Ndege cha Tanga ni mionganoni mwa viwanja 11 vya ndege vinavyofanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ufadhilli wa Benki ya Dunia kupitia *Transport Sector Support Project*.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Dunia imeonesha nia ya kufadhilli upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tanga kupitia programu iitwayo *Development Corridor Transport Programme*.

Mheshimwa Spika, kwa sasa majadiliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia kuhusu malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa mradi wa upanuzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Tanga, mapitio ya awali ya ripoti ya mradi huu pamoja na maandalizi ya taarifa mbalimbali zinazohitajika kabla ya mkataba wa mkopo kusainiwa yanaendelea.

Mheshimwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumhakikishia Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'azi Ulenge kuwa Serikali ina nia ya dhati ya kufanya upanuzi na ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Tanga. Aidha, majadiliano kati ya Serikali na Benki ya Dunia yatakapokamilika utekelezaji wa mradi huu utaanza mara moja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Parezzo swalii la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimwa Spika, ahsante, kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa fursa kama hizi mfano Ujenzi wa Mradi wa Bomba la Gesi ni fursa nzuri sana kiuchumi katika nchi na kwa kuwa Serikali imesema italipa fidia kwa ajili ya upanuzi wa uwanja huo wa Tanga, lakini je, Serikali halioni ipo haja ya dharura hata kutafuta mkopo wa dharura ili fursa hii ya ujenzi wa bomba la gesi uendane na ukarabati wa uwanja huo wa Tanga?

Mheshimwa Spika, swalii la pili, kuna mchakato pia wa upanuzi wa uwanja wa *Lake Manyara*, Karatu ambao ni uwanja muhimu sana kwa utalii katika Kanda ya Ngorongoro – Serengeti, wananchi wale hawajalipwa fidia muda mrefu.

Je, ni lini sasa Serikali italipa fidia wananchi hawa wa *Lake Manyara* pale Karatu?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa *Engineer* Msongwe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Pareoso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza naamini anakusudia kusema bomba la mafuta na si bomba la gesi; kama hivyo ndivyo Serikali inatambua umuhimu wa bomba hili na ndio maana tunapoongea hivi tayari kuna watu wanafanya tathimini kwa ajili ya watu watakaopisha upanuzi wa kiwanja hiki ili uwanja huu uendane na kasi ya utekelezaji wa mradi wa bomba la mafuta la kutoka Tanga kwenda Uganda. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Serikali inalitambua hivyo na ndio maana iko kasi kuhakikisha kwamba uwanja huu unajengwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kama amesikilliza kwenye jibu langu la msingi nimetaja viwanja 11 ambavyo viko katika mpango huu na katika kitabu chetu cha bajeti ambayo imepitishwa kiwanja cha *Lake Manyara* ni kati ya viwanja hivyo 11 ambavyo pia vinafanyika upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unafanyika hili kuweza kuhakikisha kwamba ndege sasa zinatua uwanja huu wa *Lake Manyara* kwa ajili ya kuongeza shughuli za utalii eneo hilli la Mkoa wa Manyara na Karatu kwa ujumla wake, ahsante.

**SPIKA:** Ule uwanja wa *Lake Manyara* hatari sana ule, kwa sababu unakwenda ndege inaishia hapa lile korongo gema liko hapa mbele hapa, msije mkatumbukiza ndege korongoni kule *Lake Manyara*. Mheshimiwa Zungu tafadhalii swali la nyongeza.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, mimi nakushukuru.

Mheshimiwa Spika, hii barabara inayotoka Klabu ya Yangi inapita Kata ya Jangwani na Mchikichini na kuja kuunganisha kwenye barabara ya Kawawa ni barabara ambayo inachukua magari takribani 40,000 kwa siku na hali

ya barabara hii ni mbaya, haipitiki, inaleta msongamano na kero kubwa sana kwa watumiaji wa barabara hii.

Je Serikali imechukuwa hatua gani kuboresha barabara hii?

**SPIKA:** Barabara ya kwenda Yanga hiyo shida tupu, mahandaki matupu! Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri madhira yanayowapata Yanga mengi hata barabara pia shida! Ufafanuzi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Zungu Mbunge wa Ilala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hizi alizozitaja Mheshimiwa Zungu katika moja ya vikao alitoa kama Mwenyekiti na nimempa taarifa kwamba baada ya kulisemea hilo *TANROADSM* koa wa Dar es Salaam wako *site* kuangalia barabara hii ili waweze kuikarabati na kuondoa mashimo yote ili changamoto ambaza zinatokea ziweze kuondolewa.

Kwa hiyo, ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuliahidi kwamba totalifanyia kazi tumeshalifanyia kazi na *TANROADS* Dar es Salaam wako *site* kuhakikisha kwamba changamoto ambayo ipo kwenye hizi barabara inatatuliwa haraka, ahsante.

**SPIKA:** Tunashukuru sana wapenzi wa Simba ndio wanawaombea Yanga barabara mna mapenzi makubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mrisho Gambo bado tupo hapo hapo.

Na. 494

**Changamoto ya Mafuriko – Jimbo la Arusha**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza:-

Kwa muda mrefu Jimbo la Arusha Mjini limekuwa likisumbuliwa na changamoto ya mafuriko kwenye Kata ya Sembetini, Levolosi, Osunyai, Sekei, Unga Ltd, Sakina, Baraa na Olerian yanayosababishwa na miundombinu mibovu ya barabara ya Sakina – Tengeru na *Airport* – Soko la Kilombero?

**SPIKA:** Bado tuko Ujenzi na Uchukuzi, *Engineer Godfrey Kasekenya Msongwe*, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE) alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Sakina – Tengeru umehusisha upanuzi wa barabara iliyokuwepo kutoka njia mbili kwenda njia nne na katika mito yote yamejengwa madaraja makubwa yanayopokea maji kutoka mlima Meru na kupeleka katika makorongo makubwa ya asili. Hivyo, mafuriko yanayotokea katika maeneo husika hayasababishwi na miundombinu mibovu ya barabara ya Sakina – Tengeru.

Mheshimiwa Spika, tatizo la mafuriko katika maeneo yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge yanayosababishwa na sababu zifuatazo:-

(i) Mabadiliko ya kimazingira yanayohusiana na ujenzi uliofanyika katika maeneo ya juu na hivyo kuongeza maji katika maeneo ya juu kuelekea kwenye maeneo ya chini;

(ii) Ujenzi holela katika mikondo asili ya maji na kupunguza upana wa njia ya maji; na

(iii) Utupaji taka ngumu kwenye mitaro ya maji na kusababisha kuziba kwa makalvati na kupelekea maji kupita juu ya barabara na kusambaa katika maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na tatizo la mafuriko, Serikali kupitia *Tanzania Strategic Cities Project* unaotekelezwa na Halmashauri ya Jiji la Arusha, inafanya utafiti wa kina ili kuona ni jinsi gani mafuriko haya yanaweza kuzuiwa kwa kujenga miundombinu ya kukusanya maji yote yanayotoka Mlima Meru na kuleta madhara ya mafuriko. Mhandisi Mshauri kutoka Kampuni ya *Cheil Engineering* ya Korea Kusini anaendelea na utafiti huo, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante, Mbunge wa Arusha Mjini - Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba Mheshimiwa Waziri hafahamu kwamba hii ni changamoto kubwa sana kwa Jiji la Arusha na inaathiri karibuni Kata 15 Kata ya Ulolieni, Kata ya Balaha, Kata ya Sekel, Kata ya Kimandolu, Sakina, Kaloleni, Revolosi, Sombetini Osunyai, Unga Limited, Yalelai, Daraja Mbili, Mulieti, Sokonwali na Sinoni. Unaona zaidi ya nusu ya kata zote zina changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilikuwa naomba kufahamu ni wadau gani walioshirikishwa ikiwa Ofisi ya Mbunge haijashirikishwa, nimeongea na watu wa *TARURA* hawajashirikishwa, lakini na madiwani pia wa kata zinazohusika pia awajashirikishwa; kwanza ningependa kufahamu ni wadau gani ambao wameshirikishwa kwenye hii *study* na kwenye *solution* ya hili jambo?

Mheshimiwa Spika, lakini ya pili nilikuwa naomba kwa uongozi wako kwa sababu jambo hili linahusisha Wizara mbili; Wizara ya Uchukuzi pamoja na wizara ya TAMISEMI; je, Waziri haoni haja kwamba wizara hizi mbili tukafanya kikao pale Jijini Arusha, kwa kushirikisha Mkuu wa Mkoa pamoja na Mkuu wa Wilaya ili mwisho wa siku tutafute *solution* ya kudumu kwa wananchi wetu wa Jimbo la Arusha Mjini?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri Ujenzi na Uchukuzi, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mrisho Mashaka Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi ni kwamba baada ya kupata hii changamoto ambayo mafuriko yanababishwa na maji kutoka mlimani na Mheshimiwa Mbunge amekuwa analifuutilia sana, Serikali imeamua kufanya *study* kuona namna ya kuondosha hili tatizo.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwenye *study* hii baada ya kukamilika, itakapokuwa taarifa imepatikana hatutaanza kutekeleza mradi hapo ndipo tutakaposhirikisha wadau kulingana na taarifa za *study* zitakavyokuwa zimeonyesha kwamba sasa tunategemea kufanya hiki na hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya tafiti hiyo kukamilika wadau hawa watashirikishwa kabla ya kuanza kutekeleza huo mpango ambaeo utakuwa sasa umebainika kutokana na *study* hiyo, lakini nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba sisi tulipojenga barabara hii ya *TANROADS* barabara nyngi zinazoathirika na wananchi wanaoathirika ni wa Wizara sana wanaoshughulikiwa na *TARURA* na *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge sisi kama Serikali tunafanya kazi kama timu tutaongea na *TAMISEMI* na si *TAMISEMI* tu tu pengine hata ofisi za mazingira na hata watu wa kilimo ambaeo pengine huko wanasababisha miundombinu yetu kuharibika. Kwa hiyo, nimuhakikishie Mbunge kwamba kama Serikali tunafanya pamoja kuhakikisha changamoto hii tunaiondoa, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, tunaelekeea Nishati swaliltaulizwa na Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, uliza swalilako.

Na. 495

**Umeme wa REA Vijiji 14 vya Jimbo la Manyoni Magharibi**

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka umeme katika vijiji 14 vya Jimbo la Manyoni Magharibi?

**SPIKA:** Majibu ya swalilako Naibu Waziri Nishati - Mheshimiwa Byabato Stephen Lujwahuka, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati naomba kujibu swalilako Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 14 pamoja na vijiji vingine vilivybaki katika Jimbo la Manyoni Magharibi itaanza mwezi Julai, 2021 kupitia utekelezaji wa mradi wa *REA Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili*. Mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Disemba, 2022.

Mheshimiwa Spika, kazi ya utekelezaji wa mradi huu katika Wilaya ya Manyoni kwa ujumla inahusisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 33 urefu wa kilometra 383.1, njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 urefu kilometra 31, ufungaji wa transfoma 31 zenye uwezo wa KVA 50 pamoja na kuunganisha huduma ya umeme kwa wateja wa awali 682. Gharama ya mradi ni shilingi bilioni 15.45.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aysharose swalilako nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi; pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwa kuwa Kata za Rungwa, Ipande na Kitaraka za Jimbo la Manyoni Magharibi hazina umeme kabisa jambo ambalo linakwamisha jitihada za wanawake na vijana kujikomboa kiuchumi.

Je, Serikali ina mkakati gani wa haraka wa kupeleka umeme katika umeme vijiji hivyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa vijiji vya Kinyamwenda, Itaja na Ngimu vya Jimbo la Singida Kaskazini ambavyo vilikuwa katika mpango wa mradi wa *backbone* unaoanza Singida, Arusha hadi Namanga havina umeme kabisa.

Je Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha vijiji hivi vinakuwa na umeme? Nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aysharose Mattembe kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuwa amekuwa mstari mbele sana kufuatilia upelekaji wa umeme katika Mkoa wote wa Singida na tumekuwa mara kwa mara tukijadiliana na kuhakikisha kwamba hakika tutafikisha umeme katika maeneo yote ya Kinyamwenda kama alivyosema, Kitalaka na kata nyingine ambazo ziko katika maeneo yake.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema mkandarasi anayetarajiwa kupeleka umeme katika Mkoa wetu wa Singida kwenye Wilaya yetu ya Manyoni ataanza kazi mwezi unaokuja na tutahakikisha kwamba vijiji hivyo vyote 14

ambavyo vilikuwa vimebakia bila kupelekewa umeme vinapata umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini katika swali la pili hayo maeneo mengine ambaye ameyasema yamechukuliwa na mkandarasi ambaye anapeleka umeme kutoka Iringa kupita Dodoma, Singida kwenda Arusha kwenda mpaka Namanga na viko katika *scope* yake na kazi yake inatakiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi wa saba.

Mheshimiwa Spika, tunafahamu kwamba tayari vifaa vyta kufanya kazi hiyo viro *site* kwa maana ya nguzo, waya na transforma na tutahakikisha kwamba tunasimama naye ili katika muda aliopewa aweze kukamilisha kazi hiyo ili wananchi wote wa Singida waweze kupata umeme kwa ajili ya maendeleo katika maeneo yao, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, nimekuona Mheshimiwa Kwagilwa Reuben uliza swali la nyongeza.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba kuuliza swali moja la nyongeza; ni lini Serikali itapeleka umeme kwa vijiji 28 ambavyo viko katika Jimbo la Handeni Mjini havijapata umeme mpaka sasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Handeni Mjini.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kwagilwa Mbunge wa Handeni Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimshukuru pia na yeye kwa kuendelea kufuatilia upelekaji wa umeme katika maeneo yake. Jimbo la Handeni Mjini halina tofauti na Jimbo la Bukoba Mjini ambao ni maeneo ambayo hayakuwa yananufaika na Mradi wa REA, lakini sisi tumeweka katika mradi wa *peri urban* ambao tunatarajia kuuanza mwezi wa tisa na hivyo maeneo yote ya mijini ambayo pengine bado yanaonekana yana *nature* ya vijiji; Jimbo la Bukoba Mjini,

Handeni Mjini na maeneo mengine yakiwepo yatapelekewa umeme kuanzia mwezi wa tisa kuitia mradi wetu wa *peri urban* ikiwa ni pamoja na llelma, Mwanza na maeneo kama ya Geita ambayo yako mjini, lakini yana hadhi ambayo ya kijiji. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mama Salma Kikwetu nilikuona.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana; kwanza nikupongeze wewe kwa kazi nzuri ambayo unaifanya kuelekeaa kuhitimisha Bunge letu la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, naomba niulize swalii la nyongeza, lakini kabla ya kuuliza kwanza nipongeze Serikali na Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri na kubwa inayofanya kwa sababu wakati Wizara ya Nishati inatoa taarifa yake ilisema itamalizia umeme *REA Awamu* ya *Tatu vijiji* vyote vya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, na ninataka niwahakikishie kwamba katika Jimbo langu la Mchingga wataalam wako kazini tangu tarehe 16 mwezi huu wa Juni wakiwa na mkandarasi anayeitwa *Nakuroi Investment Company Limited* wanafanya kazi nzuri sana. *Vijiji* vyote kama Kijiji cha Kiwawa, Mputwa, Ruvu na Mtamba, Luchemi, Lihimilo Mnyangala, Namkongo, Makangala na Luhoma; hivi *vijiji* vyote vimeshafikiwa, isipokuwa kuna *vijiji* viwili tu ambavyo vimesahaulika. (*Makofii*)

Nakuomba sana na ninaombaa Serikali katika awamu ile ya tatu wamalizie hivyo *vijiji* viwili ambavyo ni Kijiji cha Dimba na Kijiji cha Kitohave. Ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mama Salma Kikwete, Mheshimiwa Naibu Waziri umeshamla ng'ombe mzima imebaki mkia tu, *vijiji* hivyo una mpango gani wa kumalizia, majibu tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, nipayende kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, Mbunge wa Mchinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa shukrani kwa niaba ya Wizara, lakini na Serikali kwa Mheshimiwa Mbunge kuona kwamba Serikali kwa ujumla yake chini ya uongozi wa Mheshimiwa wa Mama Samia Suluhu Hassan imeamua kuhakikisha kwamba inawaflikishia umeme Watanzania wote mahala walipo, na kuititia mradi wa *REA* Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili kuhakikisha vijiji vyote ambavyo amekuwa amepelekewa umeme vinapelekewa.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Wabunge wengine tunafurahi kwamba sasa wakandarasi katika maeneo yetu mengi tayari wako *site*, kazi tayari zimeanza za kufanya *survey*na kuhakiki vijiji ambavyo vimechukuliwa na vitapewa umeme.

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge wale ambao katika maeneo yao hawa jawaona wakandarasi au wameendelea kupata changamoto ya mawasiliano na wakandarasi hao basi tuwasiliane ili tuweze kuhakikisha kwamba tunasimamiana ili katika muda ambao tumewahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tutapeleka umeme katika maeneo yetu, tuweze kufikisha umeme kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Waziri alisema kwamba vilikuwa vimebakvi vijiji kama 680 ambavyo havikuwa vimeingia kwenye ile awamu yetu, lakini tayari maelekezo yametolewa na vijiji vyote vilivyo katika maeneo yetu vimechukuliwa na vitafanyiwa kazi katika Awamu ya Tatu Mzunguko wa Pili bila kuacha hata kijiji kimoja.

Mheshimiwa Spika, hii ni *commitment* ya Serikali kwamba ifikapo Disemba, 2022 vijiji vyote ambavyo viko katika maeneo yetu vitakuwa vimepata umeme na kuhakikisha kwamba wananchi wote wanaendelea kufarijika

na huduma ya umeme kwa ajili ya maendeleo katika maeneo yetu nashukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Tuendelee na Kilimo sasa Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Shally Josepha Raymond Mbunge wa Viti Maalum Kilimanjaro uliza swali lako.

Na. 496

### **Kuzalisha Miche Bora ya Kahawa – Kilimanjaro**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Je, ni lini makubaliano ya kibiashara yatafanyika baina ya taasisi za umma na makampuni binafsi yanayolima kahawa Mkoani Kilimanjaro ili kuzalisha miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa na kuigawa kwa wakulima bila malipo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu kwa watu wa Kilimanjaro, Naibu Waziri Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josephat Raymond, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa miche bora ya kahawa hufanyika kupitia wakulima binafsi, vikundi vyta wakulima, Vyama vyta Ushirika, Taasisi ya Utafiti ya *TaCRI* na mikataba baina ya *TaCRI* na kampuni binafsi au shirika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na gharama kubwa ya uzalishaji wa miche hususani pale ambapo hakuna ufadhilli maalum wa taasisi au shirika, kumekuwepo na utaratibu wa wakulima kuchangia gharama kidogo ili kuwa na uzalishaji endelevu na upatikanaji wa miche bora.

Mheshimiwa Spika, mathalani wakulima hutakiwa kuchangia kiasi cha shilingi 100 kwa kila mche sawa na asilimia 10 ya gharama halisi ya mche. Kati ya Julai, 2016 mpaka 2021 *TaCRI* imezalisha jumla ya miche 2,308,606 ambayo imeendelea kusambazwa Mkoani Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, *TaCRI*/imekuwa ikiingia mikataba ya kuzalisha miche bora yenye ukinzani dhidi ya magonjwa na kuisambaza kwa wakulima kadri ya mahitaji. Mikataba hiyo ni pamoja na uzalishaji wa miche 100,000 uliofanyika kati ya mwaka 2018 na 2019 ambapo *TaCRI* ilishirikiana na *Ushiri AMCOS* ya Wilayani Rombo kuzalisha miche hiyo.

Mheshimiwa Spika, *TaCRI*/kati ya mwaka 2016 na 2019 ilishirikiana na Taasisi za Hivos na Solidaridad kutoa mafunzo kwa wazalishaji wa miche bora ya kahawa ambapo jumla ya miche 890,677 ilizalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika Wilaya za Same, Mwanga na Moshi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, nimekuona.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na kabla sijaendelea naomba nisahihishe jina langu aliviyolitamka Naibu Waziri, mimi ni Shally Josepha Raymond hakuna Josephat.

Mheshimiwa Spika, nishukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, Iakini niseme wazi kwamba ninapotamka zao la kahawa aina ya *Arabic* katika Mkoa wa Kilimanjaro ni zao dume, ni zao ambalo linawapatia wanaume kipato. Wakati zao hili linapauka, wanaume wote sasa wanakwenda kuwabana akina mama kwenye zao lao la migomba, kwenye zao lao la mbogamboga, maharage na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi niliomba kuelezwu ni nini makubaliano ya kibashara kati ya Serikali na wafanyabiashara wenye *estates*? Kwa sababu wale ndio wenye mashamba makubwa ya kahawa yanayozunguka wakulima wadogowadogo, *estates* hizo zikiwemo Tchibo, Machare, Kikafu na kadhalika.

Sasa ni lini Serikali itakubaliana na wakulima hao wa ma-estate wawasaidie hawa wakulima wadogo wadogo?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili; sina tatizo wala shida kabisa na uzalishaji wa miche kutoka *TaCRI*, lakini *TaCRI* ni kituo kimojawapo tu kinachozalisha miche pamoja na hiyo mingine aliyosema Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kufuatana na mimi mama yake, mguu kwa mguu twende katika mashamba ya wananchi tuone ambavyo zao hilo limepauka?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili kuhusu kahawa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mama Shally Raymond kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, suala la kufuatana na Mheshimiwa Mama Shally kwenda Mkoa wa Kilimanjaro, nimhakikishie niko tayari na tutapanga mimi na yeye kwa sababu nina wajibu kwake, ni mama yangu, kanilea miaka mitano nikiwa *next* kwake. Kwa hiyo, nitakwenda na nitazunguka naye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuingia mikataba na estates, kwanza mikataba ni *willingness* kati ya mtoa huduma na anayeombwa kutoa huduma, kwa hiyo, sisi kama Serikali pale ambapo watu wako tayari kuingia mikataba na Taasisi yetu ya *TaCRI* kwa gharama nafuu ambayo siku ya mwisho haitaweza kumuumiza mkulima na *conditions* ambazo haziwezi kutuumiza, tuko tayari.

Mheshimiwa Spika, lakini sasa hivi tuna programu kubwa ya kuzalisha zaidi ya miche milioni 20 ya kahawa ambayo tutaigawa katika kipindi hiki cha miaka mitano. Kwa hiyo, kwa wafanyabiashara ambao wako tayari kuingia kwa *conditions* ambazo ziko wazi na *TaCRI*, sisi wala hatuna tatizo

juu ya hilo na ndiyo maana tumetaja baadhi ya taasisi ambazo tumeshangia nazo makubaliano na baadhi ya wakulima ambao tutaingia nao makubaliano. Lakini tukienda pamoja kama tutakutana na hao wenye *estates* kubwa tutajadiliana namna ya kufanya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnes Hokororo, nimekuona; kahawa Mkoa wa Mtwara, uliza swali lako. (*Kicheko*)

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, ahsante, lakini uzalishaji wa miche ya kahawa unafanana na uzalishaji wa miche ya mikorosho iliyopo Mkoani Mtwara. Vikundi vinavyozalisha miche ya korosho Mkoani Mtwara vinaidai Serikali tangu mwaka 2018 na hivi karibuni tulipata kauli ya Serikali kwamba hundi imeandikwa.

Mheshimiwa Spika, swali langu ni je, ni lini Serikali italipa vikundi hivyo vyta uzalishaji wa miche ya korosho vilivyoko Mkoani Mtwara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo muhimu, maana vikundi hivyo hata Kongwa visto, wazalishaji nao wanataka kulipwa. Mnalipa lini Mheshimiwa Naibu Waziri?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hokororo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nitumie Bunge lako kuwaambia kwamba wakulima wadogo wote ambao walikuwa wanadai zaidi ya shilingi bilioni 1.8, tayari fedha hizi zimeshatoka na sasa tunafanya utaratibu ili Wizara ziweze kupelekwa Bodi ya Korosho na Bodi ya Korosho ianze kulipa wakulima. *Anytime* kuanzia sasa fedha hizo watakuwa wameanza kuzipata.

Mheshimiwa Spika, niwahakikishie tu kwamba kwa sababu utaratibu tuliokuwa tumejiwekea na ninashukuru Waziri wa Fedha hapa alisema kwamba taasisi yoyote ya

Serikali itakayopokea fedha dakika za mwisho, hakutakuwa na ule utaratibu wa kuzirudisha, tunaamini kwamba kati ya wiki ijayo mpaka mwanzoni mwa mwezi Julai fedha hizi zitanza kulipwa kwa sababu tayari utaratibu wake umeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile watumishi wa umma walioingia mikataba na Bodi ya Korosho, malipo yao na yenye kama Wizara sisi tumesha-*compile* na kuzipeleka Wizara ya Fedha ili na wao waweze kupata haki yao kwa sababu kuwa watumishi wa umma hakuwaondolei haki ya kulipwa kama ambavyo walitakiwa kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nimuombe Mheshimiwa Mbunge, tutaendelea kuwasiliana kwa karibu kuhakikisha kwamba mpaka Julai wakulima wote fedha zao wawe wameshazipata kwa sababu fedha hizo hata zikiingia kwetu tarehe 30 hazitarudi Hazina.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Ishengoma nilikuona, uliza swali lako tafadhali.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya zao la kahawa ya Mkoa wa Kilimanjaro yanafanana sana na matatizo ya kahawa ya Mkoa wa Kagera. Mavuno ya kahawa katika Mkoa wa Kagera huanza mwezi Aprili hadi Mei, lakini mpaka juzi Vyama vya Msingi vilikuwa havijafungua msimu wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, na tatizo kubwa liliopo hasa Wilaya ya Muleba, wananchi wanabugudhiwa na *task force* ambayo imeundwa ambayo inajumuisha watu wa PCCB, Usalama wa Taifa na watu wa Kilimo. Kila anayekutana naye anatoka shambani ana gunia moja anakamatwa na kupelekwa kituo cha polisi.

Naomba kauli ya Serikali, je, ni nini kauli ya Serikali kukomesha vitendo viovu hivi ambavyo vinawabugudhi wakulima kwa kisingizo kwamba wanalangua kahawa ilhalii wako kwenye Wilaya yao, wako kwenye tarafa yao na vijiji vyao? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Muleba Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, niseme na nirudie tena, tumefanya vikao na viongozi wa Mkoa wa Kagera, tumefanya vikao na vyama vikuu vya ushirika vya Kagera, tumefanya vikao na wanunuzi binafsi; la kwanza, hatumzuii mkulima yeoyote kupitia chama chake cha msingi kuuza mazao yake kwa mfanyakishara katika *level/ya chama* cha msingi. Hili ni jambo la kwanza, na tumeruhusu na tumetoa leseni. Na msimu umeshafunguliwa. Na wiki iliypita tulikuwa na mkutano hapa Dodoma wa wadau wote wa kahawa.

Mheshimiwa Spika, la pili, tuwaombe viongozi katika ngazi za Halmashauri na Wilaya. Sekta ya kilimo haiwezi kusimamiwa kimabavu, sekta ya kilimo inasimamiwa kwa misingi ya *win-win*. Mkulima anayevuna mazao yake kutoka shambani kuyapeleka kwenye nyumba yake ama kuyapeleka kwenye chama chake cha msingi, naomba kupitia Bunge lako niwaombe viongozi walioko katika Halmashauri na Wilaya wasiwabughudhi.

Mheshimiwa Spika, lakini haturuhusu vilevile wafanyakishara wanaowafuata wakulima mashambani kwenda kununua mazao chini ya bei ya soko, halafu wao kupeleka kwenye minada na Chama cha Msingi ili waweze *ku-benefit* na bei. Hilo hatutaruhusu na wala hatutaruhusu mfanyakishara yeoyote anayechepusha mazao kuvusha kwenye mpaka wa Tanzania na Uganda.

Mheshimiwa Spika, tunawataka na nitumie Bunge lako kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kama mna wanunuzi kutoka Uganda ambao wana uwezo wa kutupa bei nzuri, waleteni Wizarani tutawapa leseni, watakwenda kununua katika mfumo rasmi bila kubugudhiwa na mtu yejote.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mmabo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika ya Mashariki. Swali litaulizwa na Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya.

Na. 497

### **Diplomasia ya Uchumi Kupitia Meli ya MV Mbeya II**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha biashara kupitia Diplomasia ya Uchumi kati ya Tanzania na Malawi kwa kutumia meli ya MV Mbeya II?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambao ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Balozi Mbarouk tafadhalii.

### **NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, meli ya MV Mbeya II yenye uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 za mizigo ilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 5 Januari, 2021. Meli hii kwa sasa inafanya safari kati ya Bandari za Tanzania tu za Kyela na Mbambabay.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sera ya Diplomasia ya Uchumi ni mionganoni mwa majukumu makubwa ya Wizara yangu. Kutohana na umuhimu mkubwa wa kukuza biashara kati ya Tanzania na Malawi na katika kuhakikisha kuwa meli ya MV Mbeya II inatumika ipasavyo, Ubalozi wa Tanzania nchini Malawi, ukishirikiana na Mamlaka ya Bandari Tanzania (*TPA*) imeanza mawasiliano na Serikali ya Malawi na taasisi zake kupitia Wizara ya Mambo ya Nje ya Malawi ili kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha MV Mbeya II kufanya safari zake nchini Malawi.

Mheshimiwa Spika, ubalozi wetu uliopo Lilongwe, Malawi pia unafuatilia kwa karibu kufikia makubaliano (*MoU*) baina ya Serikali ya Tanzania na Malawi kuhusiana na uanzishaji wa Ofisi za *TPA* mjini Lilongwe ambazi zitasimamia utekelezaji na uendeshaji wa shughuli zote za kibashara zinazotumia huduma za bandari za Tanzania. Hii inatokana na maazimio ya Marais wa Tanzania na Malawi wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais wa Malawi nchini Tanzania iliyofanyika tarehe 7 - 8 Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa taratibu hizo na kukamilika kwa kipindi cha majoribio ya meli hiyo na hivyo kuanza safari zake nchini Malawi, ni dhahiri kuwa biashara kati ya Tanzania na Malawi kwa kutumia Ziwa Nyasa italmarika. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyanya tafadhalii.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa kuwa imethibitika kwamba Wilaya ambazo ziko mpakani zinanufaika sana kupitia biashara na majirani zao wa nje, na kwa kuwa katika Wilaya ya Nyasa, kwanza kuna uasilia wa kindugu lakini vilevile kuna changamoto kubwa za kukuza biashara na Malawi ingekuwa ni mkombozi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameonesha kuwa na uwezo mkubwa wa kidiplomasia kwa jinsi ambavyo amenijibu swalı langu, namshukuru sana, je, Waziri una mpango gani wa kwenda kuongeza nguvu ya kupeleka ushawishi katika nchi ya Malawi?

Mheshimiwa Spika, swalı la pili, kwa kuwa...

**SPIKA:** Ushawishi wa nini?

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ushawishi wa kuhakikisha kwamba suala hilo ambalo tumelizungumzia la kibashara linafanyika kwa kutumia meli na nyenzo nyingine.

Mheshimiwa Spika, swalı la pili, ninapenda pia kumualika Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri kuja Wilaya ya Nyasa ili kuwafahamu wananchi wa kule na shughuli wanazozifanya na kuona namna bora zaidi ya kukamilisha kushughulikia suala hili la kibashara. (*Makof*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo tafadhalni na mwaliko huo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer Stella Manyanya*, Mbunge wa Nyasa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki itafanya kila jithada kwa kushirikiana na mamlaka husika nchini Malawi ili kuwezesha meli ya MV Mbeya II ianze safari zake kati ya Malawi na Tanzania pale taratibu zote zitakapokamilika. (*Makof*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu swalı la pili ambao ni mwaliko, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge

kwamba nitakuwa tayari, kwa idhini yako, kufanya safari hiyo ili kuona fursa mbalimbali ambazo ziko katika Wilaya ya Nyasa. Ahsante sana. (*Makofî*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Balozi Mbarouk Nassor Mbarouk, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje.

Swali la mwisho kwa siku ya leo linakwenda Wizara ya Fedha na Mipango na litaulizwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza. Mheshimiwa Shonza tafadhali.

Na. 498

**Changamoto ya Msongamano wa Magari  
Mpaka wa Tunduma**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE K.n.y. MHE. JULIANA D. SHONZA** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kutatua changamoto ya msongamano wa magari yanayovuka kuelekea nchi jirani kupitia mpaka wa Tunduma?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa *Engineer* Masauni tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari katika Kituo cha Forodha Tunduma. Hatua hizo ni pamoja na kutekeleza mpango wa kurasimisha utaratibu wa kubadilishana taarifa za mizigo kati ya Dar es Salaam na Nakonde, Zambia; kuendelea kutoa huduma za forodha kwa muda wa saa 24; kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya pande

mbili ili kuwezesha taarifa za mizigo inayotoka katika Bandari ya Dar es Salaam kwenda Zambia kusomana kwa wakati; na kufuatilia kwa karibu utekelezaji wa makubaliano baina ya pande mbili ya Januari, 2020 kuhusu mkakati wa kuboresha miundombinu ya barabara pamoja na ujenzi wa maeneo ya maegesho ya magari kwa upande wa Zambia.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Zambia zitaendelea kuimarisha utendaji wa taasisi zote zinazohusika na shughuli za forodha katika Kituo cha Tunduma, pamoja na kuboresha mifumo ya TEHAMA na miundombinu ya barabara ili kukabiliana na changamoto ya msongamano wa magari.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa hii nafasi.

Mheshimiwa Spika, msongamano huu wa magari katika Mji wa Tuduma haujaathiri tu magari yanayopita mpakani, lakini umeathiri wananchi na usafiri wa daladala, na wananchi wote hata wanaokwenda mikoa ya jirani. Lakini Mheshimiwa Rais, Marehemu Dkt. Magufuli, alipofika wakati wa kampeni aliahidi kilometra 10 za lami kwa ajili ya kupunguza huu msongamano kwa ajili ya kujenga njia za pembezoni na za mchepuko. Sasa nini kauli ya Serikali kuhusu ahadi hii ya Mheshimiwa Rais alioitoa ya kilometra kumi za lami ili kupunguza msongamano katika Mji wa Tunduma? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha naomba kujibu swali la nyongeza la

Mheshimiwa George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tunakubali kwamba ahadi hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais. Lakini kwa kutambua changamoto ya msongamano ambayo ipo pale Tunduma, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi ina mambo yafuatayo ili kuondoa hizo changamoto za msongamano.

Mheshimiwa Spika, kwanza, tunategemea kubadilisha mfumo wa mizani iliyopo iwe ni *weigh in motion* ambayo inachukua muda mfupi sana, pale Mpemba ambayo ni jirani, kama kilometra 10 pale Tunduma, ambayo inachukua takribani dakika moja mpaka mbili gari linakuwa limeshapita. Kwa hiyo, itakuwa ni moja ya njia za kuondoa msongamano.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, nitumie Bunge hili kusema kwamba Halmashauri ya Tunduma waweze kuongeza maegesho ili magari ambayo hayaendi kwenye Kituo cha Forodha yasiwe na sababu ya kukaa barabarani. Kwa hiyo, ni fursa kwa Halmashauri ya Tunduma kuongeza maegesho.

Mheshimiwa Spika, mkakati wa tatu, ile barabara sasa hivi tunaifanya utaratibu tuweze kupanua njia ili kuwe na *lane* badala kuwa na *lane* mbili ziwe walau ziwe hata *lane* nne, lakini mkakati wa nne ni kutengeneza *bypass* ya barabara ili magari yote ambayo yanakwenda ama yanatoka yaani yanakwenda Mkao wa Rukwa na Mkao wa Katavi hadi Kigoma yasiwe na sababu ya kupita Tunduma, kwa hiyo yapite pembedi ili kuruhusu hii barabara sasa iwe huru na tunaamini tukifanya hivyo tutakuwa tumepunguza sana msongamano katika njia hii. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naona Mheshimiwa David Silinde anatamani aulize swali la nyongeza hapa. (*Kicheko*)

Msongamano kule Namanga, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, tafadhali.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swalii dogo la nyongeza kwenye suala hili la msingi lillolenga Wizara ya Fedha.

Katika mpaka wa Namanga kuna tatizo kubwa sawa la Tunduma la msongamano wa magari ambayo wakati mwingine huchukua hata zaidi ya siku tatu yakingojea kuwa *cleared* yaweze kuendelea na safari na adha kubwa inayotokea ni kwamba hakuna miundombinu ya vyoo, mahali pa kuoga wale wanaokaa kwenye malori na wanachafua sana mazingira.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha kwamba wakati mipango ya kutengeneza maeneo sahihi ya kuengesha haya malori na sisi Longido tuna sehemu *TANROADS* wametenga zaidi ya hekari 200 na ujenzi unaendelea, wana mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wa mipakani hawapati magonjwa ya mlipuko kwa sababu ya msongamano wa magari na hakuna miundombinu ya kijamii?

**SPIKA:** Bado tupo kwako Mheshimiwa Naibu Waziri kama ulikuwa unamsikiliza maswali yake, majibu tafadhali, msongamano wa Namanga.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, naomba nimuhakikishie Mheshimiwa wa Jimbo la Longido kwamba Serikali inazifahamu hizo changamoto na tupo kusaidiana na wenzetu, sisi ndiyo tunaojenga vile vituo tunayatambua hayo na tutahakikisha katika mpango wa karibu tunakwenda

kuondoa hizo changamoto ikiwa ni pamoja na kujenga hiyo miundombini ya haraka ili wananchi wasiweze kupata adha ikiwa ni pamoja na kuangalia utaratibu wa kupunguza ile misongamano kwa kujenga barabara na maegesho makubwa ili magari yatakayokuwepo kwenye foleni ni yale tu ambayo yanatakiwa kwenda kwenye Vituo vya Forodha, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana, tumemaliza kipindi cha maswali, nianze na matangazo baadaye nitatambulisha wageni.

Waheshimiwa Wabunge Wanawake wa CCM mnaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa kikao cha kawaida cha Baraza Kuu la UWT kitakachofanyika tarehe 26 Juni, 2021 kuanzia saa tatu asubuhi katika ukumbi wa *NEC* Dodoma. Mgeni Rasmi atakuwa ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi.

Kuna tangazo kwamba leo Ijumaa tarehe 25 Juni, 2021 baada ya kuahirisha Bunge kutakuwa na semina kuhusu Mfuko wa Barabara na umuhimu wa matengenezo ya barabara nchini. Semina hiyo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa, semina itaendeshwa na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi. Kwa hiyo Waheshimiwa tukitoka hapa tunaenda kwenye semina ambayo utaratibu wake umekaa vizuri. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawatangazieni kwamba kesho tarehe 26 Juni kutakuwa na mechili ya kirafiki ya mpira wa miguu na mpira wa pete kati ya *Bunge Sports Club* dhidi ya Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) michezo yote itafanyika katika viwanja vya *College* ya *Informatics* kuanzia saa kumi alasiri kule *UDOM*.

Wageni wengine ni wageni maalum kabisa hawa ni wageni wa Mheshimiwa Waziri Mkuu ambao ni wagenu 36 hii ni timu ya *Ruangwa Queens*. (*Makofi*)

Naomba msimame *Ruangwa Queens*, hawa wapo kwenye ligi ya daraja la kwanza hapa Dodoma na jana

wameifunga Njombe Jiji goli moja, hongereni sana, hongereni sana na Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa mnamuona na anafanya kazi nzuri sana na ndiyo kiongozi wetu hapa Bungeni, hongereni sana Wana Ruangwa, muwapelekee salaam huko, huko Ruangwa kwa wingi. Ahsante sana, ahsante. (*Makofi/Kicheko*)

Golikopa wa timu hii naomba asimame huyu anaitwa Manula, huyu anadaka kweli kweli, hongera sana golikipa wetu. Haya *Bunge Queens* kama kweli mnajiweza hebu fanyeni utaratibu muone mtakavyopigwa magoli na *Ruangwa Queens*, naona mmebonyea kimya *Bunge Queens*, karibuni sana tumefurahi sana kuwa nanyi, karibu sana. (*Makofi/Kicheko*)

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, ni wageni 36 wa Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani - Waziri wa Nishati ambao ni Wanakwaya wa KKKT kutoka Chato, Mkoani Geita wakiongozwa na Ndugu Abia Gikanka. Wale Wanakwaya kutoka Chato, karibuni sana, karibuni sana, sana wanakwaya hivi Chato nao wanajua kuimba kweli ndiyo leo nasikia jamani. Hongereni sana na karibuni sana tungekuwa hapo nje tungesema m-tune kidogo tuone, ahsante sana. (*Kicheko*)

Tuna wageni 21 wa Mheshimiwa George Mwenisongole ambao ni Wakuu wa Shule za Msingi kutoka Mbozi, Mkoani Songwe wakiongozwa Mwalimu Mathias Joseph. Wale walimu, karibu sana, karibuni sana, sana, karibuni sana Dodoma, karibuni sana Bungeni, tumefurahi na tunafarijika kuwa nanyi, karibuni sana. (*Makofi*)

Kwa kweli kwa Dodoma kwa upande wa utalii wa ndani Bunge letu linaongoza kwa kuleta Watanzania Bungeni, kabisa, kabisa na tuzidi kuwaalika Watanzania wengine waendelee kujiardaa kwa Mabunge yanayokuja ni vizuri kutembelea Bunge lenu na kuweza kuona namna gani Bunge linafanyakazi siyo unapiga kura tu halafu Mbunge anaenda wapi hupajui, tunawakaribisheni sana. (*Makofi*)

Wageni 40 wa Mheshimiwa Aloyce Kamamba ambao ni wapigakura wake kutoka Kakonko, Mkoo wa Kigoma wakiongozwa na Agnes Malinzi. Wale wa Kankoko, jamani, jamani, karibuni sana, karibuni sana, karibuni Wayungu, hawa wanaitwa Wayungu hawa maana kutoka Jimbo la Buyungu karibuni sana. Wametoka mbali kweli kweli, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara na mtoto wake Ndugu Bernard Lubogo, Onesphorus Lubogo na Ndugu Cynthia Lubogo, karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Anne Malecela, ooh huyu namruka hajaja.

Wageni 20 wa Mheshimiwa Priscus Tarimo, ambao ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha *UDOM* wanaotoka Moshi Mkoani Kilimanjaro, wakiongozwa na Juma Omary. *UDOM* karibuni sana *UDOM*, karibuni simameni tuwaone, basi karibuni sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wanne wa Mheshimiwa Jacqueline Kainja ambao ni ndugu zake kutoka Urambo Mkoani Tabora wakiongozwa na wifi yake Ndugu Zabibu Mkamba. Karibuni sana, karibuni sana Wanyamwezi ninyi angalieni magari mengi mjini hapa, karibuni sana. (*Makofi/Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Florent Kyombo ambaye ni Kada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Misenyi, Ndugu Gisela Banyenda, ahsante sana (*Makofi*)

Wageni 20 Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, ambao ni walimu na wanafuzi wa shule ya sekondari ya Kwafilosa kutoka Iringa wakiongozwa na Mkuu wa shule Ndugu Dario Gakala. Karibuni sana wa Iringa, watoto wetu karibuni sana sana kutoka Iringa. (*Makofi*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Timothy Mnzava, wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Korogwe Vijijiini. Wale wa *UDOM* wanaotoka Korogwe, karibuni sana, wapo pale juu kabisa, karibuni sana, sana. (*Makofi*)

Wageni 26 wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi amba o ni wanafunzi wa vyuo vikuu mbalimbali wakiwa hapa Dodoma wanaotoka Morogoro wakiongozwa na Reuben Kitungu, wale wa Morogoro wanaosoma Vyuo Vikuu vya Dodoma, karibuni sana pia, karibuni. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Rashid Shangazi, amba o ni Viongozi wa Dini ya Kiislamu kutoka Mkoani Tanga Hassan Shedafa, Mohamed Hamis na Hillal Yunus, karibuni sana, wale pale, karibuni sana, sana, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Sanga kutoka Dodoma, Veronica Noti na Issa Ally, karibuni wale pale. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Shukrani Manya, amba o ni marafiki zake Martha Ngwenya, Kelvin James na Louis Sebyiga, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Nicholaus Ngassa kutoka Dar es Salaam Godfrey Surera, karibu Godfrey. (*Makofi*)

Wageni 16 wa Mheshimiwa Jafari Chege, amba o ni wapigakura wake kutoka Rarya, Mkoani Mara, karibuni sana kutoka Rarya, inathibisha jinsi nilivyosema Bunge linatembelewa kutoka maeneo mbalimbali, maana tumepata toka Kankoko, kutoka Rarya, kutoka Kyela kila mahali nchini wanakuja, karibuni sana. Tunaamini Rarya kule mmetuletea kamongo. (*Kicheko*)

Mgeni wa Mheshimiwa Yustina Rahhi ambaye ni mdogo wake kutoka Hanang Ndugu Daniel Tsere, karibu sana Daniel. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Ndaisaba Ruhoro, ambao ni Wasanii kutoka Dar es Salaam, Hassan Yagga na Gladness Kifaruka, karibuni wasanii. (*Makofi*)

Wageni 28 wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga ambao ni wanakwaya wa Waadventista kutoka Nzihi, Mkoani Iringa wakiongozwa na Yolanda Kavenuke. Wale Waadventista Wasabato kutoka Iringa karibuni sana sana, karibuni sana ndugu zangu. (*Makofi*)

Wageni 71 wa Waheshimiwa Rose Tweve na Cosato Chumi ambao ni wanakwaya ya Mtakatifu Cecilia kutoka Mafinga Mkoani Iringa wakiongozwa na Ndugu Dickson Mwipopo. Cecilia, hongereni sana sana, karibuni sana sana leo Iringa imetia fora, karibuni sana Mtakatifu Cecilia, tumefurahi sana kuwa nanyi. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Dkt. Rita Kabati, ambao ni ambao ni wanafunzi wa *UDOM* wanaotoka Iringa wakiongozwa na Omary Gandaga, karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni sita wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni wanafunzi wa *UDOM* Gidius Kato, Emmanuel Mlay na Mary Hassan, karibuni sana, popote pale mlipo. (*Makofi*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Boniphace Butondo ambao ni Madiwani kutoka Kishapu, Mkoani Shinyanga, Mheshimiwa Richard Kasanzu na Mheshimiwa Lameck Nsubata. Madiwani karibuni sana. (*Makofi*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben ambao ni familia yake kutoka Handeni Mkoani Tanga wakiongozwa na Mke wake Odilia Kasiga, ahsante sana karibuni sana, Mama Kwagilwa hatujakuona bado, usimame tena. Anatoka Handeni Mjini huyo, haya bwana. (*Makofi*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam; Hamisi Pele, Ahmed Ngahemela na Sabri Balagash, karibuni sana. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Mwantumu Zodo, Ndugu Mujibu Wandi, karibu Mujibu. (*Makofii*)

Wageni watatu wa Mheshimiwa Augustine Vuma, Ndugu Simon Malando, Martin Malando na Mathayo Nyanda, karibuni sana popote pale mlipo. (*Makofii*)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Assa Makanika ambaao ni ndugu zake kutoka Marekani; Regina Helus na Olivia Kasihwaki, karibuni sana, karibuni sana. (*Makofii*)

Kwa mafunzo; wageni 50 kutoka Kanisa la Wasabato Nyamazobe la Nyegezi, Jijini Mwanza wakiongozwa na Augustine Musalamba, wale nafikiri wataingia baadaye sababu *gallery* zimejaa, wapo wapi? Okay karibuni sana, karibuni sana watani zetu. (*Makofii*).

Wageni 30 kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii kilichopo Jijini Dar es Salaam, Chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam, karibuni sana Chuo cha Ustawi wa Jamii, karibuni Dodoma, karibuni Bungeni na ahsante sana. (*Makofii*)

Wageni watano kutoka Dodoma hapa hapa wakiongozwa na Lucy Kamugisha, karibuni sana. (*Makofii*)

Kuna mgeni kutoka hapa hapa Dodoma ambaye ni Ndugu Yusuph Ong'era, karibu sana Ong'era. (*Makofii*)

Wageni wawili kutoka Dodoma hapa hapa Anna Mbarouk na Monica Mbarouk, ahsante. (*Makofii*)

Wageni wawili kutoka Jijini Dar es Salaam ambaao Ndugu Mary Massawe na Glory Monyo. (*Makofii*)

Huo ndiyo mwisho wa matangazo na wale wanafunzi wa *UDOM*wanaotoka jimbo la Mchinge naomba msimame, karibuni sana, karibuni sana sana. Karibu, ahsante. (*Makofii*)

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo wa Spika, tuendelee.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76 kuomba mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, jana tarehe 24 Juni wakati nauliza swalii la nyongeza kutokana na swalii la msingi namba 488 la Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu, niliuliza swalii kutaka kujua mgawanyo wa zilizokuwa mali ya Jiji la Dar es Salaam. Kwa bahati mbaya sana moja ya vyombo vyaa habari viliripoti vibaya swalii hilo na kuandika Mheshimiwa Chaurembo amehoji juu ya kuvunjwa kwa Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, chombo hiki kwa kweli kimenifadhaisha sana, kimeniletea magomvi na baadhi ya Wabunge wenzangu wanaotokana na Jiji la Dar es Salaam, lakini pia kimenifadhaisha nakunisababishia kujihisi kama kinataka kunichonganisha na chama changu pamoja na Serikali yangu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako.  
*(Makofii)*

**SPIKA:** Naomba jambo hili tulichukue kama meza tutafanya ufuatillaji wa jambo hili, lakini kwa ujumla tukupe pole sana na tuwaambie Wabunge wa Dar es Salaam kwamba ndugu yetu hakuwa na nia hiyo ambayo mnaifikiria na niviase tu vyombo vyaa habari, muwasikilize vizuri Wabunge, muwatendee haki badala ya kupotosha potosha taarifa kwa lengo maalum na hata tukimwambia atueleze hapa ni chombo gani utakuta ni vyombo vile ambavyo vina nia mbaya. *(Makofii)*

Kwa hiyo, vyombo vyaa habari tuwe makini sana na hasa mitandao yetu pia. Serikali wenzetu mitandao imekuwa ni mahali ambapo watu wanafikiri wanaweza kumdhaliilisha mtu yeyote, wanaweza wakafanya chochote, hili eneo lina matatizo sana. Kwa mfano pia jana kuna tangazo fulani

lilitoka la majina mengi kwamba limetolewa na *TRA* katika majina yale mengi ya Wizara mbalimbali yapo na majina ya Wabunge wa Bunge la Kumi na Moja liliomiliza muda wake, nafikiri mliliona Waheshimiwa kwenye mitandao huko.

Kumbe lengo lao kumfuatilia mtu mmoja tu wanayemtaka wao kuonyesha kwamba ana madai fulani Bungeni, lakini orodha imetolewa ndefu na wakaanza kumshambulia Spika mle na kuchonganisha na kadhalika.

Niseme tu kwa wote walioguswa tangazo hilo ni la uongo, ni tangazo lilikuwa la mwaka 2018 huko nyuma na malipo hayo yalisharekebishiwa na niwaambie Wabunge ambaao wamemaliza muda wao maana yake wengine hali mbaya huko. Sasa walipoona lile tangazo simu ya Spika imejaa bwana tuna madeni tunadai kwako, hakuna anayedai Bunge, hakuna, hakuna. Katika chombo ambacho kinafanya kazi vizuri kimojawapo ni Bunge jamani, kweli kabisa. (*Makofi*)

Mbunge awe ni Mbunge wa Upinzani sijui wa wachache, sijui wa wengi, hakuna anayedai. Awe aliyekuwepo, aliyekuwepo kabla ya kabla, hakuna anayedai na kama mtu ameishiwa huko Ulaya au wapi si aseme tu kuliko kusingizia Bunge kila wakati kwamba kuna madai. Hakuna anayedai, hayupo na hata huyo mtu wao alilipwa kila kitu, ila malipo yake yalipokwenda Benki, Benki walichukua zote. (*Makofi/Kicheko*)

Unajua watu wengine wanataka kila wakati mje na vitu kumuumbua mtu, kwa nini mnaamini amini vitu ambavyo havipo! Bunge ni moja ya chombo ambacho hakimuonei mtu, kama mtu ana madai yoyote unafuatwa utaratibu, hakuna shida. Bunge haliko hivyo, hatujawahi kuwa hivyo sisi hata siku moja, hatumuonei mtu kwa sababu sijui ametoka wapi au imekuwaje hapana hatufanyi hivyo. (*Makofi*)

Kwa hiyo, wale wa mitandao tunaomba sana mlipe heshima Bunge na kama mtu mmoja ana mambo yake hayo ni mambo yake na anapaswa kufuata *channel* zilizopo ili

kutatua. Na upande wa Serikali haidaiwi chochote katika lile tangazo, ni tangazo la zamani na lilishakuwa *sorted* zamani hizo halituhusu hivi sasa wala halipo. Hata Wizara ya Fedha nadhani tangazo lao ni hivyo kwamba ni la zamani na si la sasa, maana ni la 2018. Walichofanya kwenye tangazo lile hawajaweka tarehe, halafu wanalitoa mara kwa mara.

Kwa hiyo shida hii sio ya kwako Chaurembo peke yako inatusumbua watu wengi sana *misinformation* katika nchi yetu. Halafu watu wanaondoka *scot-free*, anachanganya umma, hafanywi chochote, halafu siku nyingine tena hafanywi chochote. Tena wengine wanajiita Mchungaji sijui nani nani yaani unashangaa kabisa. Lakini huko mbele tunavyozidi kwenda baadhi yao tutaanza kuwaita, Kamati yetu ya Maadili iko pale pale, tumevumilia ya kutosha. (*makofi*)

Baadhi yao tutaanza nao sasa kwenda nao sambamba maana yake tunakaribia kuchoka, hii hali ya kupakana pakana matope kusikokuwa na mbele wala nyuma. Tunaomba wajue Taasisi ya Bunge ina namna ya *kuji-defend* wawe makini sana na taarifa zinazohusu Bunge hasa za upotoshaji. (*Makofi*)

Katibu.

#### **NDG. JOSHUA CHAMWELA- KATIBU MEZANI:**

#### **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

Muswada wa Sheria kwa ajili ya kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali zipatazo 14 kwa lengo la kuondoa mapungufu ambayo yamejitokeza katika sheria hizo wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo (*A Bill for An Act to Amend Certain Written Laws*).

(*Kusomwa Mara ya Kwanza*)

**SPIKA:** Ahsante. Tumepata Hati ya Dharura kutoka kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano - Samia

Suluhu Hassan ya kututaka tushughulikie sheria ambazo ziko katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Namba 3 wa mwaka 2021 na ni muhimu kwa sababu ni sheria zinazorekebishwa zinazoendana na uwekezaji wa bomba la mafuta la kutoka Uganda. Kwa hiyo, linagusa sekta mbalimbali ili kuwezesha uwekezaji huo kuweza kwenda vizuri bila matatizo yoyote na sisi Wabunge mnafahamu tuna-*support* kabisa mradi huo. Kwa hiyo, tutauhughulikia muswada huu kwa hatua zake zote katika kipindi hiki hiki cha Bunge kabla hatujaondoka hapa.

Kwa hiyo, Muswada huo tutaujadili siku ya Jumatano wiki ijayo, siku ambayo ndio tutaujadili Muswada huo baada ya maswali, tukimaliza Muswada huo ndio Mheshimiwa Waziri Mkuu, atasimama kusoma hotuba ya kuahirisha Bunge hadi wakati mwingine. (*Makofi*)

Sasa Muswada huo una sheria mbalimbali zinazohitaji marekebisho, utakuwa kwenye Kamati ya Katiba na Sheria. Lakini kwa sababu ni sheria mbalimbali zinagusa sekta mbalimbali za nishati, za uchukuzi, za mambo ya barabara na kadhalika, nimeteua Wabunge ambao wataungana kutoka kamati mbalimbali ambao wataungana na Kamati ya Katiba na Sheria na wataanza kuushughulikia leo leo huo muswada na siku zinazoendelea ili *by* Jumatano ya wiki ijayo tuweze kuuingiza humu ndani na tuweze kuusoma. Naamini Katibu mtauweka kwenye *tablets* za Waheshimiwa Wabunge.

Kutoka Kamati ya Sheria Ndogo ambao nimewateua wajunge na Kamati hiyo ya Katiba na Sheria, ni Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Mheshimiwa Judith Kapinga, Mheshimiwa Ramadhan Suleiman Ramadhan, Mheshimiwa Sylvia Francis Sigula na Mheshimiwa Priscus Jacob Tarimo. (*Makofi*)

Kamati ya Miundombinu ni Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka na Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila. (*Makofi*)

Kamati ya Nishati na Madini ni Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo, Mheshimiwa Nusrat Shaaban Hanje na Mheshimiwa Stella Martin Manyanya. (*Makofi*)

Na Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, maana yake kuna Sheria za Serikali za Mitaa ambazo nazo zitaguswa na bomba hili ni Mheshimiwa Humphrey Hesron Polepole, Mheshimiwa Abdallah Jafari Chaurembo, Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta. (*Makofi*)

Hao watajiunga na Kamati ya Katiba na Sheria ili kuweza kuweka sawa mambo haya na wengine tunaruhusiwa siku moja moja kupita pita huko kuona nini kinachoendelea, ila usidai mambo mengine yanayohusu utaratibu. Ahsante.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU MEZANI:**  
Uchaguzi wa Wajumbe kwenye Taasisi mbalimbali.

### **UCHAGUZI**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama inavyoonekana kwenye *Order Paper* ya leo, Ijumaa tarehe 25 Juni, 2021 kutakuwa na Uchaguzi wa Wajumbe kwenye Taasisi mbalimbali kupitia rasmi sasa hapa Bungeni. Uchaguzi huu unafanyika kwa kuwa nafasi za uwakilishi katika vyombo au taasisi mbalimbali zenyе uwakilishi wa Bunge zimebaki wazi baada ya Bunge la Kumi na Moja liliokuwa mwaka 2015/2020 kuvunjwa mwaka jana.

Nafasi zilizopo ni Tume ya Utumishi wa Bunge, Bunge la Afrika, Jukwaa la Mabunge ya Jumuia ya Maendeleo ya Afrika ya Kusini mwa Afrika kwa maana ya *SADC-PF*, Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*) na Umoja wa Maziwa Makuu (*Great Lakes*).

Kanuni ya 14 na Nyongeza ya Pili ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020 kwa ujumla wake inaelekeza kwamba Uchaguzi wa Wabunge wanaokwenda katika vyombo vingine ambavyo kwa mujibu wa mikataba au sheria zinazounda vyombo hivyo, vinatakiwa viwe na wawakilishi wa Bunge utafanywa kwa kuzingatia kwa kadri iwezekanavyo uwiano wa idadi ya Wabunge wa vyama vyaa siasa vyenye uwakilishi Bungeni, uwakilishi wa jinsia na pande mbili za Muungano na kwa kuzingatia utaratibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Wabunge hao uliowekwa katika Nyongeza ya Pili ya Kanuni za Bunge.

Kama nilivyowatangazia tarehe 7 Juni, 2021 kwamba Wabunge wenye nia ya kugombea nafasi za uwakilishi wapeleke majina yao kwenye ofisi za vyama, hivyo basi majina yaliyopokelewa na kupendekezwa kujaza nafasi hizo yanatoka kwenye kambi husika na *caucus* husika.

Sasa kwa kuwa idadi ya wagombea waliojitokeza kwa maana ya majina tuliyoyapokea rasmi ni sawasawa na idadi ya nafasi zilizopo, maana wangkuwa ni wengi kuliko idadi ya nafasi maana yake tungefanya chaguzi kwa kupiga kura. Lakini idadi ya majina yaliyokuja ni sawasawa na idadi inayotakiwa. Katika mazingira kama hayo wagombea hawa watapita moja kwa moja bila kupingwa, lakini kwa taratibu zetu nitalihoji Bunge ili muweze kulithibitishia, kama hawa wagombea mnawapitisha rasmi au vinginevyo. (*Makofii*)

Kwa hiyo, nitawataja majina halafu nitawahoji mnaoafiki na msioafiki. Majina niliyoyapata kwa upande wa Tume ya Huduma za Bunge ambayo Mwenyekiti wake ni Spika, Makamu Mwenyekiti ni Naibu Spika na Waziri wa Nchi tunaingia moja kwa moja kwa sababu ya ile sheria. (*Makofii*)

Wajumbe wanaoongezeka hapo sasa kuunda Tume ya Bunge wanaopendekezwa, ni Mheshimiwa Aeshi Khalfan Hilaly, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Janejelly James Ntate, Mheshimiwa Zahor Mohammed Haji,

Mheshimiwa Fakharia Shomar Khamis, Mheshimiwa Halima James Mdee na Mheshimiwa Khalifa Mohamed Issa. (*Makofii*)  
Sasa nawahoji wanaoafiki kwamba hawa wawe Wajumbe wa Tume waseme ndio, wasioafiki waseme sio.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. (*Makofii/Kicheko*)

Tunakwenda Bunge la Afrika (*PAP*) wawakilishi ni watano, ninawasoma watano hao; Mheshimiwa Ng'wasi Damas Kamani, Mheshimiwa Toufiq Salim Turky, Mheshimiwa Jerry William Silaa, Mheshimiwa Nape Moses Nnauye na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest. (*Makofii*)

Wanaoafiki waseme ndio, wasioafiki waseme sio.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. (*Makofii*)

Kwa hiyo, watano hao ndio wawakilishi wetu kwenye chombo hicho cha *PAP*.

Kwenye *SADC-PF*, Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, Wajumbe wake ni wanne na watano Mheshimiwa Shally Raymond. Hawa wanne wanaoungana na Mheshimiwa Shally Raymond ni Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea na Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga. (*Makofii*)

Wanaoafiki waseme ndio, wasioafiki waseme sio.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki. (*Makofii*)

Umoja wa Mabunge Duniani (*IPU*), Umoja huu Wabunge wengi humu ndani hawaufahamu. Umoja wa

Mataifa (*UN*) inayo-wing Geneva ambayo wing hii ndio inashughulikia habari ya Mabunge yote duniani, *actually* hili ndio Bunge kubwa Duniani, maneno mengisana humu ndani huwa *PAP, PAP, PAP* hakuna cha *PAP* wala nani, *IPU* ndio kiboko yao na hata mikutano yake ni mikubwa sana na inahusisha sio tu Wajumbe hawa, lakini na Maspika wote Duniani, ambao wanahudhuria na basi mengine tutazidi kuelezana. Kwa miaka ijayo mahali pa kuomba ni *IPU*sio huko kwingine. (*Makofi/Kicheko*)

Waliopita kwenye eneo hilo ambao wanapendekezwa ni Mheshimiwa *Engineer Mwanaisha Ng'anzi Ulenge*, Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani, Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mheshimiwa Elibariki Immanuel Kingu na Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko. (*Makofi*)

Wanaoafiki hawa wawe Wajumbe wetu waseme ndio, wasioafiki waseme sio.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote wameafiki, nawashukuruni sana. (*Makofi*)

Umoja wa Maziwa Makuu (*Great Lakes*), mapendekezo ni Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa *Engineer Ezra John Chiwelesa*, Mheshimiwa Deus Clement Sangu na Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba. (*Makofi*)

Wanaoafiki waseme ndio, wasioafiki waseme sio.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Basi wamechaguliwa.

*(Wabunge walijotajwa walipitishwa na Bunge Zima kuwa Wajumbe katika Tasisi Mbalimbali)*

**SPIKA:** Nawashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge.

Kwa maana hiyo sasa *process* yetu ya Uchaguzi wa hizi nafasi zote imekamilika na hawa tuliovataja na kuwapitisha humu Bungeni ndio watakuwa wawakilishi wetu. (*Makofi*)

Niwakumbushe kule mnakoenda hamuendi *in your own individual capacity*, mnaenda mkituwakilisha sisi na mkiwakilisha Watanzania. Kwa hiyo, kabla hujasimama ukasema chochote, lazima ujiulize kwanza hiki kitu kina maslahi na nyumbani? Kama una wasiwasi una-*cross check* na sisi kwa sababu dunia siku hizi mawasiliano ni *faster*, ni dakika tu, tunakupatia kila kitu unachotaka kusema. Tunakupa hata *notes*, tunakuletea *comments*, tunaomba watu wa Wizara ya Mambo ya Nje chapuchapu wanaku-*assist*, kama unahitaji jambo fulani au mjadala fulani na kadhalika. (*Makofi*)

Msiende huko mkaanza kusema ya kwenu, mko huru kabisa msiseme kama Spika amewafunga, mko huru kabisa, ili mradi katika ajenda zile ambazo mnaona kidogo zinahitaji kuwa na umuhimu mnafanya hivyo.

Lakini la pili na muhimu Kanuni zetu tumezibadilisha, mkizisoma na itakuwa ni vizuri mjisome kuhusu wawakilishi wetu katika vyombo vya nje. Tulipata taabu mtakumbuka kwenye Bunge lililopita na baadhi ya Wajumbe walituletea shida kule, tulirekebisha Kanuni. Kwa hiyo, tuna uwezo sasa Kikanuni wa kuku-*recall*, wa kukuita kutoka huko uliko hata katikati ya Mkutano, ukarudi hapa Maadili na hatua zikachukuliwa. (*Makofi*)

Mwanzioni Kanuni zetu hazikuwa na hiyo *provision* kwa sababu tulikuwa hatuna tatizo lolote, lakini tulipopata matatizo haya ikabidi Kanuni zikae sawasawa. Kwa hiyo, bado wewe ni mwakilishi wetu.

Mwisho, wawakilishi wetu ninyi hao ni Wabunge wa Bunge la Tanzania, hiyo ndio kazi yako ya kwanza na unawajibika hapa kwa kila kitu *including* sisi kukuwezesha kwenda kwenye mikutano yako hiyo na kurudi ni sisi hapa, kwa hiyo, unawajibika hapa. Baadhi yao hudhani sasa kwa kuwa tumewachagua hapa wana wajibika kule. Kule unakwenda sawa, lakini uwajibikaji wako ni hapa na tutataka *progress reports* ili baadaye ziende kwenye Kamati ya Mambo ya Nje kuona ni kitu gani kinachoendelea tuweze kwenda pamoja. (*Makof!*)

Kwa sababu mtakapoenda huko tutakuwa tunawapa na Makatibu wa Bunge ambao wanafuatana na nyinyi ambao watakuwa wanaandika zile ripoti mnazipitia, mna-*submit* kwa Spika ili tuweze kuwa na muendelezo. Kama kuna jambo la muhimu limepatikana huko tunawasambazia Waheshimiwa Wabunge wote waweze kujua nini kinachoendelea huko. Tunawapa wenzetu Serikalini na wao waweze kujua kinachoendelea huko inakuwa ni jambo jema sana.

Basi baada ya hilo na maelezo hayo kuna wageni wa Mheshimiwa, Mwantumu Dau Haji wa kutoka Kusini Unguja wapo sita, naomba msimame. Ahsanteni sana, wageni wetu toka Kusini Unguja, karibuni Dodoma na mimi kichama ndio mlezi wenu huko Kusini Unguja, kwa hiyo, karibuni sana karibuni sana Dodoma. Tunawashukuruni sana. (*Makof!*)

Basi baada ya hapa kwa kuwa mambo ni mengi na Waheshimiwa naandaa andaa mambo yenu, kwa ajili ya kuijandaa kuondoka Dodoma wiki ijayo, basi natoa muda huu muweze kufanya hivyo na kesho tumetangaza kuna semina. Siku ya Jumatatu itakuwa ni ratiba ya Kamati ya Sheria Ndogo itatoa taarifa yake humu Bungeni siku ya Jumatatu tutajadili hilo.

Siku ya Jumanne kama ratiba haitabadiika, Serikali itakuwa inazindua Mpango wa Miaka Mitano, kwa hiyo, baada ya maswali tutaenda kwenye uzinduzi wa Mpango

ambao kazi itakayoongozwa na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango na siku ya Jumatano kama nilivyosema tutakuwa na hii sheria na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuahirisha shughuli za Bunge. (*Makof!*)

Basi kwa hatua hiyo na kama nilivyooleza tukitoka hapa tunakwenda Msekwa, kuna mambo ya barabara na kadhalika ambayo nayo yameandalowi vizuri. Kwa hiyo, mtaona tuko *busy* kwa kipindi hiki kilichobakia, ningombaa tuendelee kuwa pamoja mpaka siku ya Jumatano tutakapoahirisha shughuli zetu.

Kwa hatua hiyo basi naomba niahirishe shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu ijayo saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 4:40 Asubuhi Bunge Lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 28 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)*